Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | September-2026

EAJK

Mbinu za Lugha Katika Mikakati ya Mawasiliano Kwenye Mahakama ya Mazingira na Ardhi, Kisumu

Authors

Eddah Martha Njeri [1]; Beverlyne Asiko Ambuyo [2]; Deborah Nanyama Amukowa [3]

Main author's email: eddahmartha@gmail.com

(1.2.3) Maseno University, Kenya.

Cite this article in APA

Njeri, E. M., Ambuyo, B. A., & Amukowa, D. N. (2026). Mbinu za lugha katika mikakati ya mawasiliano kwenye mahakama ya mazingira na ardhi, Kisumu. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, 5(1), 192-200. https://doi.org/10.51317/shj6j930

OPEN ACCESS

A publication of Editon Consortium Publishing (online)

Article history

Received: 2026-07-12
Accepted: 2026-08-15
Published: 2026-09-21

Scan this QR to read the paper online

Copyright: ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

Ikisiri

Lengo la makala hii ni kuchunguza utendaji wa mbinu za lugha ndani ya mikakati ya mawasiliano katika kesi za mizozo kwenye Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu, na jinsi mwingiliano huo huathiri mawasiliano katika mahakama hii. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Ujihusishaji kama ilivyoendelezwa na Giles et al. (1991) ambayo ilitumika kuchambua namna washiriki katika mawasiliano ya mahakama hufanya mabadiliko ya kimaongezi katika mbinu za lugha kupitia dhana za makutano na mwachano katika mawasiliano ili kuimarisha maelewano au kuchochea mizozo ya kimawasiliano. Data ilikusanywa kwenye Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu. Utafiti ulilenga mawasiliano ya kesi sita zilizokuwa zimeratibiwa kusikizwa katika mahakama hii mwezi wa Oktoba 2019, ambapo sampuli ya kesi nne iliteuliwa kimakusudi kati ya hizo kwa kuwa ziliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili. Mbinu ya uchunguzi usio wa kushiriki ilitumika katika kukusanya data. Baada ya data kukusanywa, ilipangwa kisha kuchanganuliwa kupitia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Makala hii imebainisha kwamba mawakili, hakimu na walalamishi katika mahakama hii hutumia lugha kwa njia ambayo huathiri mchakato mzima wa upatikanaji wa haki. Makala hii ilichunguza namna lugha inavyotumika kama chombo cha utatuzi wa mizozo kulingana na mbinu za lugha zilizotumika. Matokeo yanabainisha kuwa mbinu za kuchanganya na kubadili lugha pamoja na takriri ziliashiria makutano yaliyoimarisha maelewano baina ya washiriki nayo maswali balagha yakajitokeza kama mbinu ya mwachano iliyochochea migogoro ya kimawasiliano mahakamani.

Maneno muhimu: Mahakama, mbinu za lugha, migogoro, mikakati ya mawasiliano, ujihusishaji.

UTANGULIZI

Mawasiliano katika miktadha ya kitaasisi hususan katika mahakama huongozwa na kanuni kali za kisheria pamoja na taratibu za kimahakama ambazo huathiri mchakato mzima wa utatuzi wa mizozo. Ili kufanikisha mawasiliano katika mazingira haya, wahusika ambao ni majaji, mawakili, washtakiwa, mashahidi na hata walalamishi hulazimika kujipanga kimawasiliano kwa kutumia mikakati ya mawasiliano kwa njia itakayowawezesha kuwasilisha ushahidi na kujibu hoja za upande mwingine kwa uwazi na ufasaha. Hata hivyo, ufanisi wa mikakati hii ya mawasiliano hutegemea jinsi washiriki wanavyotumia mbinu mahususi za lugha kama urudiaji, maswali balagha na kuchanganya na kubadilisha lugha ili kujenga mazingira ya kirafiki ya kuwasiliana. Hii ina maana kwamba, uchunguzi wa uhusiano wa dhana hizi katika mchakato wa mawasiliano mahakamani utaweza kutoa uelewa mpana kuhusu ufanisi wa mchakato wa upatikanaji wa haki.

Katika muktadha wa mawasiliano ya mahakamani, uhusiano baina ya mikakati ya mawasiliano na mbinu mbali mbali za lugha hubainika kupitia jinsi washiriki wanavyotumia lugha ili kutekeleza majukumu yao ya kimawasiliano. Kwamba, lugha inayotumiwa katika kutekeleza mikakati kama kuuliza maswali na kukatiza usemi hususan na majaji na mawakili huku mashahidi, washtakiwa na walalamishi wakitumia usimulizi hudhihirika kupitia mbinu za lugha ambazo huchangia katika kuelekeza mwelekeo wa mawasiliano. Isitoshe, shughuli hizi huibua matumizi ya lugha kulingana na malengo, majukumu na nafasi ya wahusika katika mchakato wa kesi ambayo huathiri utekelezwaji wa mikakati ya mawasiliano.

Tafiti mbali mbali zimechunguza matumizi ya mikakati ya mawasiliano na mbinu za lugha katika mawasiliano ya utatuzi wa mizozo mahakamani. Kwa mfano, Kiguru (2014) na Aldosari (2024) walichunguza matumizi ya mkakati wa maswali na kubainisha kuwa, kando na kutumiwa kama chombo cha ushawishi na uwasilishaji wa ujumbe, mawakili hutumia maswali kudhibiti mwelekeo wa maingiliano na kudhihirisha tofauti za kimamlaka baina yao na washiriki wengine. Kwa upande mwingine, mbinu za lugha za lugha zimetafitiwa ili kubainisha dhima yake katika mawasiliano mahakamani. Owiti (2019) amechunguza mbinu mbali mbali za kimtindo na kipragmatiki kama vile tasfida, upanuzi wa maana na ulainishaji wa maneno; ambazo hutumiwa na wakalimani pale mahakamani na kuonyesha namna wanavyoweza kubadilisha au kupoteza maana halisi ya kisheria wanapotafsiri. Isitoshe, imebainishwa kwamba maswali ya balagha hutumika kama nyenzo kuu ya ushawishi katika muktadha huu (Alkabiri, 2024).

Kimsingi, mwelekeo wa tafiti hizo za awali katika uwanja wa uchanganuzi wa mazungumzo ya mahakamani umesalia katika kuchunguza dhana za mikakati ya mawasiliano na mbinu za lugha kama vipengele vinavyojitegemea. Kwa sababu hii, kutenganishwa kwa dhana hizi kunazua changamoto ya kuelewa jinsi mbinu za lugha huendesha mikakati ya mawasiliano katika utatuzi wa mizozo. Kwamba, ingawa mikakati hii ni muhimu katika kuwasilisha ushahidi pamoja na kudhibiti mwingiliano baina ya washiriki, ni dhahiri kuwa itafanikiwa kuleta matokeo yaliyokusudiwa iwapo itahusishwa moja kwa moja na mbinu mahususi za lugha maana ndizo zinazoipa uhai kiutendaji. Isitoshe, kando na kujenga taswira ya mawasiliano yanavyoendesha mahakamani, muungano wa dhana hizi utasaidia kuelewa jinsi wahusika hushirikiana na kutangamana kimawasiliano licha ya tofauti za kimamlaka baina yao. Kwa misingi hii, utafiti huu ulichunguza namna mbinu za lugha zilivyoendesha mikakati ya mawasiliano katika mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya Jiji la Kisumu.

Jiji la Kisumu ni mojawapo ya miji inayoshuhudia ongezeko la migogoro ya ardhi hususan kutokana na shughuli za kiuchumu na ukuaji wake (Obange & Wagah, 2019). Hili limeifanya mahakama ya Mazingira na Ardhi katika jiji hili kuwa muktadha unaofaa katika kuchunguza mbinu za lugha zinavyotumika ndani ya mikakati ya mawasiliano ili kuwasilisha ushahidi mahakamani.

MAPITIO YA MAANDISHI

Tafiti zilizoangazia matumizi ya lugha mahakamani zilitegemea sana nadharia ya Uchanganuzi Usemi iliyoasisiwa na kuendelezwa na Fairclough (1989). Fairclough anasema kwamba matumizi ya lugha hayawezi kutenganishwa na jamii ambamo mawasiliano hutokea. Kwa sababu hii, nadharia hii inaiona lugha kama kitendo cha kijamii ambacho hujenga mahusiano ya mamlaka, itikadi na utawala.

Kupitia mtazamo wa nadharia hii, tofauti za kimamlaka baina ya wazungumzaji katika mawasiliano ya kesi mahakamani zimechunguzwa. Tofauti hizi zimebainishwa kudhihirisha udhibiti ambao hutekelezwa kupitia mkakati wa maswali na majibu ya nadharia hii.

Katika mazingira ya mahakama, mtazamo wa nadharia hii unaweka msingi wa kuelewa matumizi ya lugha mahakamani kwa kuwa mawasiliano katika muktadha huu huhusisha wahusika wenye mamlaka tofauti kama vile hakimu, wakili, washtakiwa na walalamishi. Hivyo, matumizi ya mikakati ya mawasiliano pamoja na mbinu za lugha inaweza kuelezwa kwa kuihusisha na mahusiano yao katika mchakato wa mawasiliano mahakamani.

Isitoshe, kwa kuwa mawasiliano katika mahakama hutegemea lugha katika ujenzi na uwasilishaji wa ushahidi, michakato yote ya mahakama hutekelezwa kupitia lugha (Gibbons, 2003; Cotterill, 2003). Hivyo, washiriki katika mawasiliano hayo hutumia mikakati ya mawasiliano kama vile maswali, usimulizi na ukataji kauli ili kutawala mwingiliano (Drew & Heritage, 1992). Kwa mtazamo huu, mbinu za lugha kama vile takriri, kuchanganya na kubadilisha lugha pamoja na maswali balagha si dhana zinazojitegemea bali ni rasilimali kuu zilizofumbatwa ndani ya mikakati ya mawasiliano na huchangia katika udhibiti wa masimulizi mahakamani na kuonyesha misimamo ya wahusika (Heffer, 2005). Hivyo basi, uchanganuzi wa mawasiliano mahakamani unahitaji muundo uliounganisha na kuoanisha mbinu za lugha moja kwa moja na mikakati ya mawasiliano.

Kwa kurejelea mahakama nchini Kenya, kunazo tafiti zilizochunguza matumizi ya lugha katika mazingira haya kwa mitazamo tofauti. Kiguru (2014) alitumia muundo wa kimaelezo na mbinu za kithamano kupitia uchambuzi wa sauti zilizorekodiwa za mahakama ili kuchunguza namna maswali na matendo ya kiusemi yalivyoashiria mgawanyiko wa kimamlaka baina ya washiriki wakati wa uchunguzi wa moja kwa moja na uchunguzi wa maswali ya kukanusha. Utafiti wake ulibainisha kwamba lugha ya mahakamani hutumiwa kama nyenzo kuu ya kujenga mahusiano ya kimamlaka baina ya washiriki katika mchakato wa mazungumzo mahakamani. Aidha, Omwancha et al. (2024) walichunguza uzingatiaji wa kanuni za ushirikiano katika mawasiliano ya mahakamani na kubaini kuwa kanuni hizo huzingatiwa katika hatua za uchunguzi na mawakili. Utafiti wao ulibainisha kwamba washiriki huteua miundo maalum ya maneno ili kufikia malengo yao ya kimawasiliano. Hata hivyo tofauti na tafiti hizi, utafiti huu utaonyesha muungano wa mikakati ya mawasiliano na mbinu za lugha katika mahakama ya Mazingira na Ardhi ya jiji la Kisumu.

Misingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na misingi ya nadharia ya Ujihusishaji kama ilivyoendelezwa na Giles et al. (1991). Nadharia hii inaeleza kwamba wahusika katika kikundi fulani cha mawasiliano hufanya mabadiliko katika namna wanavyotumia lugha kulingana na muktadha wa mazungumzo. Waliangazia zaidi muktadha wa mawasiliano baina ya wasemaji na kusema kuwa ndio huchochea kuwepo kwa mabadiliko katika mtindo wa mazungumzo. Hii inaonyesha kwamba, wanenaji hufanya mabadiliko ya kimaongezi kulingana na muktadha wa mazungumzo pamoja na malengo yao ya kuwasiliana. Nadharia hii iliufaa utafiti huu kwani ilisaidia katika kuchunguza ujihusishaji ambao hujitokeza kupitia mbinu za lugha katika mawasiliano kwenye mahakama.

Nadharia hii vile vile imeainisha aina mbili za Ujihusishaji: Ujihusishaji wa makutano na Ujihusishaji wa mwachano. Giles et al. (1991) wanabainisha Ujihusishaji wa makutano kama njia ya ushirikiano na utangamano wa kijamii. Kwamba, makutano ni namna ambavyo wazungumzaji hubadilisha njia za kujieleza ili kudhihirisha ushirikiano na utangamano wao kupitia usemi, ishara au mabadiliko ya kimaongezi. Kwa mujibu wa wataalamu hawa mtu fulani anaweza kuamua kuacha jambo fulani kwa hiari yake ili aimarishe mawasiliano kati yake na anaowasiliana nao. Kwa upande mwingine, Ujihusishaji wa mwachano kwa mujibu wa Giles et al. (1991), ni mbinu ambapo wanakikundi hufanya mabadiliko ya kimaongezi kwa kujitenga na washiriki wengine katika kikundi cha mawasiliano. Hapa, mnenaji anaweza kujitenga kutegemea nia yake katika mawasiliano. Ikumbukwe kwamba msemaji anaweza kuwa na makutano katika kiwango kimoja na mwachano katika kiwango kingine.

Vipengele vya lugha, muktadha na utambulisho vya nadharia hii vilitumika kuchanganua kauli za washiriki zilizohusisha mbinu za takriri, maswali balagha na kuchanganya na kubadilisha usemi. Mbinu hizi

zilichunguzwa kwa kuzihusisha na mikakati ya mawasiliano ili kubaini jinsi zilivyochangia ujihusishaji wa makutano na mwachano miongoni mwa washiriki wa mawasiliano. Hivyo, misingi ya nadharia hii ilitoa msingi wa kuchunguza namna mawakili, hakimu, walalamishi, washtakiwa na mashahidi katika kesi za mizozo kwenye mahakama walivyojihusisha.

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulikuwa wa kithamano kwani ulilenga kuchunguza na kueleza data ambayo haikuwa ya kitakwimu kwa kuzingatia maana na muktadha wa mawasiliano yaliyochunguzwa. Muundo wa kiuchanganuzi ulitumiwa ili kumwezesha mtafiti kuchanganua kwa kina data ya mawasiliano ya kesi kwenye mahakama hii. Utafiti ulifanywa katika Mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya jiji la Kisumu. Mahakama hii iliteuliwa kwani ndiyo mahakama maalum inayosikiza na kutoa maamuzi yanaohusiana na kesi za migogoro ya mazingira na ardhi hivyo. Kundi lengwa lilikuwa kesi sita ambazo zilikuwa zimeratibiwa kusikizwa katika mwezi wa Oktoba 2019 kwenye mahakama hii.

Kipindi hiki kiliteuliwa kwa kuwa data ya utafiti ilikusanywa katika mwaka huo, hivyo kiliwakilisha taarifa zilizopatikana katika mahakama hii wakati wa kufanywa kwa utafiti huu. Sampuli ya utafiti ilikuwa kesi nne za migogoro ya umiliki wa ardhi ambazo ziliteuliwa kwa kutumia usampulishaji wa dhamira maana ziliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili na pia zilitengewa muda mwingi wa mawasiliano ikilinganishwa na vikao vinginevyo. Kesi mbili zilizobaki zilitengwa maana mawasiliano yake yaliendeshwa kwa lugha ya Kiingereza ilhali utafiti huu ulilenga kuchanganua mawasiliano ya kesi yaliyoendeshwa kwa lugha ya Kiswahili.

Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchunguzi usio wa kushiriki ambao ulimwezesha mtafiti kushuhudia mambo yeye mwenyewe na kumwezesha kurekodi mawasiliano namna yalivyoendeshwa. Utafiti ulitumia uchanganuzi wa yaliyomo ili kuchanganua data ambapo mawasiliano ya kesi yaliyokuwa yamenaswa yalinukuliwa kisha kuchujwa kwa kutumia orodha ya uchunzaji ili kubainisha mbinu za lugha ndani ya mikakati ya mawasiliano. Orodha hii iliandaliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na misingi ya nadharia ya Ujihusishaji. Data iliwasilishwa kwa njia ya kimaandishi na kuambatanishwa na nukuu halisi za mawasiliano kati ya wahusika kisha kuchanganuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Ujihusishaji (Giles et al., 1991).

Maadili ya utafiti yalizingatiwa ambapo mtafiti alipata idhini ya kufanya utafiti kutoka vitengo vilivyohusika. Pia mawasiliano ya kesi yaliyorekodiwa na kunakiliwa yalihifadhiwa vyema na mtafiti ili kuzuia matumizi yasiyoidhinishwa. Ili kulinda siri za washiriki pamoja na vipande vya ardhi vilivyohusika, mtafiti alitumia nambari pamoja na herufi za kialfabeti ili kulinda utambulisho wao. Isitoshe, data iliyokusanywa ilitumika kwa minajili ya utafiti huu pekee.

MATOKEO YA UTAFITI

Matokeo ya utafiti yalidhihirisha matumizi ya mbinu tatu za lugha katika mawasiliano ya kesi za migogoro ya ardhi katika mahakama ya Mazingira na Ardhi ya jiji la Kisumu. Mbinu hizo ni pamoja na takriri, kuchanganya na kubadilisha lugha pamoja na maswali balagha. Aidha, mbinu hizi zilibainika kutumika ndani ya mikakati ya mwasiliano. Mbinu hizi zilichambuliwa kwa kuzingatia nadharia ya Ujihusishaji (Giles et al., 1991) na kuonyesha namna wahusika walivyokutana au kuachana katika mawasiliano. Sehemu inayofuata inajadili mbinu hizi kwa kutumia dondoo halisi kutoka mahakamani.

Mbinu ya kuchanganya na kubadili lugha imebainishwa kujitokeza mara kwa mara katika mawasiliano hasa wazungumzaji wanapotumia lugha tofauti kwa muda (Binyanya, 2014). Washiriki katika mawasiliano kwenye mahakama walichanganya na kubadili lugha kupitia matumizi ya lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Kiluo. Mfano wa matumizi ya mbinu hii katika hatua ya mahojiano ya upande pinzani:

> *Wakili: Ndio nasema ulileta objection?*
> *Mlalamishi: Mimi sikuleta objection.*
> *Wakili: Hukuleta objection?*

Hapa, mawasiliano haya yamo katika hatua ya mahojiano ya upande pinzani ambapo wakili anamhoji mlalamishi kuhusu iwapo aliwasilisha pingamizi la kisheria mahakamani. Wakili anatumia mkakati wa maswali na kushirikisha istilahi ya Kiingereza *objection* ndani ya swali lililoulizwa kwa lugha ya Kiswahili. Istilahi *objection* ni moja kati ya istilahi nyingi ambazo

hutumika katika sajili ya kisheria kwa hivyo matumizi yake yanaashiria uhusiano uliopo kati ya uchaguzi wa lugha na mahitaji ya muktadha wa kimahakama. Vile vile, wakili anapopata jibu la kukataa kutoka kwa mlalamishi anarudia kuuliza dhana ile ile lakini kwa njia nyingine tofauti huku akiendeleza kuchanganya lugha. Kwamba, swali la pili *'Hukuleta objection?'* linaonekana kutafuta ufafanuzi wa jibu la mlalamishi pasi na kulenga kutafuta taarifa huku likisisitiza ushahidi uliokuwa unatolewa. Usisitizaji huu unafanyika kupitia mbinu ya kuchanganya lugha.

Isitoshe, wahusika walibadilisha lugha kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiluo kisha baadaye kurejea katika lugha ya Kiswahili kwenye hatua hiyo ya mahojiano ya upande pinzani ambapo mawakili waliwahoji walalamishi kama ifuatavyo:

> *Mlalamishi: (Anasema kwa lugha ya Kiluo) Puodhoni en mara.*
> *Wakili: Si utumie Kiswahili? Hii shamba ilikuwa imesajiliwa kwa jina la marehemu X? X ni nani kwako?*
> *Mlalamishi: Ni ndugu yangu.*

Hapa, hali ya mlalamishi kubadilisha lugha ya matumizi na kujibu swali kwa lugha ya Kiluo naye wakili kuendelea kumhoji kuhusu suala la mmiliki wa shamba kwa lugha ya Kiswahili inaonyesha kuwepo kwa ubadilishaji wa lugha hizi mbili katika mfululizo huo wa mawasiliano.

Swali la wakili *'Si utumie Kiswahili?'* linatokea mara tu baada ya mlalamishi kutumia Kiluo kama njia ya kusisitiza kuhusu lugha inayofaa kutumika katika mazungumzo yao; huku maswali yanayofuata kwa lugha ya Kiswahili yakilenga kupata ushahidi kuhusu mmiliki wa shamba.

Wakati mwingine, kupitia mkakati wa mazungumzo mawakili walibadili lugha kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza walipozungumza moja kwa moja na hakimu. Kwa mfano:

> *Wakili: Sawasawa. Ni sawa X. That will be all my Lord. That marks the close of the plaintiff's case.*

Hapa, wakili anaanza mazungumzo kwa Kiswahili akimrejelea mlalamishi kisha anabadilisha kwa lugha ya Kiingereza hususan akimlenga hakimu. Mabadiliko haya ya lugha yanafanyika katika hatua ya kufungwa kwa ushahidi wa mlalamishi na yanaonyesha namna mawakili hutumia lugha mahususi kulingana na wahusika mahususi wanaolengwa katika mawasiliano mahakamani.

Matokeo yanaonyesha kuwa mabadiliko ya kimaongezi yaliyojitokeza kupitia mbinu ya kuchanganya na kubadili lugha yametumiwa kama rasilimali kuu ya kimawasiliano katika mkakati wa maswali na mazungumzo. Matokeo haya yanapanua kidogo mawazo ya Binyanya (2014) ambaye alitazama mabadiliko haya kama sifa ya kawaida ya sajili ya maafisa wa polisi ambayo yalichangia katika kuleta ushirikiano baina ya wazungumzaji katika kituo cha polisi. Kwamba, ingawa taasisi za vituo vya polisi na mahakama zimo chini ya mfumo mmoja wa sheria na utekelezwaji wa haki, uhuru wa wahusika wa kuchanganya na kubadili lugha katika muktadha wa mahakama hupungua na kubadilika kwa sababu ya ugumu wa lugha ya kisheria na nia ya msemaji katika mawasiliano. Katika utafiti huu matumizi hayo yalibainika ndani ya mikakati ya mawasiliano ya maswali na mazungumzo katika mazingira ya mahakama. Mabadiliko haya ya msimbo yanaweza kutafsiriwa kwa kuzingatia nafasi ya lugha katika kujenga utambulisho wa mhusika na mahitaji ya mawasiliano katika muktadha huu.

Kwa mujibu wa Giles et al. (1991), wahusika wanaweza kufanya mabadiliko ya kimaongezi ili kujihusisha kwa kukutana. Giles wanayaona makutano kama njia ambazo huwawezesha wawasilianaji kutangamana, kukuza ukaribu na hivyo kurahisisha mwingiliano. Ujihusishaji wa makutano unaweza kufafanuliwa kwa kuzingatia vipengele vya lugha, muktadha na utambulisho vya nadharia hii. Kwanza, mawakili pamoja na walalamishi wanafanya uteuzi wa lugha ya kutumia kati ya Kiswahili, Kiingereza na Kiluo ili kujieleza katika mwingiliano huo. Hii ina maana kwamba, uteuzi huo wa lugha na wahusika hawa ulikuwa kipengele cha ujihusishaji.

Katika dondoo la kwanza, wakili anapoanzisha matumizi ya neno *objection* kisha mlalamishi kurekebisha uteuzi wake wa lugha ili uafikiane na ule

wa wakili ni ishara kwamba washiriki hawa wanajihusisha kwa kukutana. Mbinu ya kubadilisha na kuchanganya lugha katika maongezi haya inaonyesha unyumbufu wa lugha miongoni mwao hali inayowawezesha kukuza ushirikiano.

Pili, tendo la wakili la kubadili lugha na kuzungumza na hakimu kwa Kiingereza linaweza kutafsiriwa kama ujihusishaji wa makutano kwani ni mabadiliko ambayo yanajitokeza kulingana na muktadha rasmi wa mahakama na utambulisho wa kitaaluma baina yao kama wahusika katika mfumo wa kisheria.

Vile vile, mbinu ya takriri ilibainika kutumika kupitia mkakati wa maswali ambapo washiriki walirudia maneno au kauli mbali mbali kama ilivyo katika dondoo lifuatalo:

> *Wakili: Babako ako wapi kama ni babako?*
> *Mlalamishi: Amekufa.*
> *Wakili: Amekufa. Eleza mahakama shamba imesajiliwa kwa jina la nani. Kwa jina la baba ama kwa jina la...*
> *Mlalamishi: (Kimya)*
> *Wakili: Jibu!*
> *Mlalamishi: Ushataja majina mengi mimi hapana jua.*
> *Hakimu: Jibu swali ulililoulizwa!*
> *Wakili: Nimekuuliza shamba imesajiliwa kwa jina lako ama la baba yako?*
> *Hakimu: Shamba liko kwa jina la nani?*

Dondoo hili linahusu mahojiano baina ya wakili na mlalamishi na yanajitokeza katika hatua ya mahojiano ya upande pinzani, ambapo wakili katika kesi hii anamhoji mlalamishi. Wakili anarudiarudia neno *amekufa* baada ya mlalamishi kulitumia katika jibu lake. Aidha, hakimu anarudia kauli *jibu swali* kama njia ya kumwelekeza mlalamishi kwenye swali analohitajika kujibu. Urudiaji huu unaashiria kuwa takriri haikutumiwa kwa ajili ya kusisitiza kauli pekee bali kama njia ya kuelekeza mawasiliano pamoja na kuweka wazi matarajio ya mahakama kwamba mshiriki anahitajika kujibu hoja alivyoulizwa badala ya kutoa taarifa.

Kwa mtazamo wa nadharia ya Ujihusishaji (Giles et al., 1991) huu ni ujihusishaji wa makutano ambapo kwa kuzingatia kipengele cha lugha katika nadharia hii, wakili hachagui neno linginelo la kurudia bali anahiari kurudia neno lililokuwa limetumiwa na mlalamishi ili kuwa karibu naye kimatumizi na hivyo kupunguza umbali wa kilugha. Isitoshe urudiaji huu katika muktadha wa mazungumzo kati ya wakili na mlalamishi unawawezesha kuendelea kushiriki katika hoja ile ile na hivyo kuimarisha mawasiliano.

Isitoshe, hakimu anaporudia kauli *'Jibu!'* na *'Jibu swali ulililoulizwa!'* hafanyi hivyo ili kumkandamiza mlalamishi bali anafanya hivyo kwa kutumia utambulisho wake ili kuokoa mawasiliano yaliyokuwa yanaelekea kufeli. Kwamba, anadhihirisha ujihusishaji wa makutano kwa kurudia muundo wa amri wa wakili ili kutilia mkazo hitaji lile lile la lugha ambalo lingefungua njia ya maelewano kuhusu kinachotafutwa ambacho ni mmiliki wa shamba.

Kwa mujibu wa Aldosari (2023) maswali yanapoulizwa kwa ajili ya kumshurutisha mjibu maswali mahakamani hufanywa hivyo ili kuzuia mchipuko wa maelezo yasiyohitajika. Hili linabainika zaidi hakimu anaporudia swali na istilahi kama njia ya kumwelekeza mlalamishi kwenye taarifa mahususi anayohitajika kueleza kulingana na mahitaji ya muktadha huu wa mawasiliano. Kwa hiyo, uchanganuzi wa data aidha umeonyesha kwamba mbinu ya takriri ilitumika na mawakili na hakimu kama njia ya kutangamana kimawasiliano. Matokeo haya yanatofautiana na utafiti wa Nabirye (2012) anayejikita katika kutazama mbinu ya urudiaji kama chombo cha ukandamizaji na ujenzi wa tofauti za kimamlaka baina ya washiriki ambao ni wataalamu wa kisheria na washiriki wa kawaida wasio na utaalamu huo. Nabirye anasema kuwa mawakili hawatumii mbinu ya takriri kwa kubahatisha tu bali huitumia ili kuwachanganya mashahidi na kudhihirisha kwamba mawakili ndio wenye mamlaka ya kutawala mawasiliano mahakamani. Hata hivyo, hii haina maana kwamba utafiti wa Nabirye haukutambua umuhimu wa mbinu ya takriri katika mawasiliano mahakamanai. Tofauti na mtazamo wake, utafiti huu sasa umebainisha mtazamo chanya unaothibitisha kwamba mbinu ya takriri inaweza kuwakutanisha wazungumzaji na kuimarisha mwingiliano wao wa kimawasiliano kupitia mkakati wa maswali.

Mbinu ya maswali balagha pia ilibainika kutumika katika mahakama. Mbinu hii ilibainika katika matumizi

ya mikakati ya maswali pamoja na mahojiano. Mbinu hii ilitumiwa na washiriki wa mawasiliano katika hatua ya mahojiano ya upande pinzani kama ifuatavyo:

> *Wakili: Umeshitaki watu watano. Kina nani umeshitaki kwa hii kesi?*
> *Mlalamishi: Sijui majina yao.*
> *Wakili: Huwezi kumbuka majina yao? Lazima ujue mwenye umeshitaki. Si wewe ndiwe umeleta hii kesi mbele ya mahakama? Wewe ndiwe umeleta hii kesi mbele ya mahakama. Hujui hata mmoja mwenye umeshitaki kwa hii kesi?*

Katika dondoo hili, wakili anatumia swali la kukanusha *'Si wewe ndiwe umeleta hii kesi mbele ya mahakama?'* kama swali balagha. Katika mawasiliano ya mahakamani, maswali balagha ni maswali ambayo huwa hayatafuti majibu mapya bali yana malengo mahususi yanapotumika. Kwa hivyo, swali la kukanusha analouliza wakili linabainisha jibu linalotarajiwa kwamba ni mlalamishi mwenyewe aliyeleta kesi. Swali la wakili linaweza kuchambuliwa kama swali balagha linalobeba ajenda ya wakili mwenyewe na hivyo linamjenga wakili kama mjenzi mkuu wa simulizi za ushahidi hasa mlalamishi anapolemewa kimawasiliano katika hatua hii ya kesi.

Hautli-Janisz et al. (2022) japo hawakutafitia mazingira ya mahakamani, wanaibua maoni kwamba wazungumzaji wanaoshiriki midahalo hutumia maswali balagha katika kuwasilisha madai yao pasi na kutarajia majibu ya mdomo kutoka kwa mzungumzaji mwingine. Kwa misingi hii, wakili katika dondoo hili hatumii swali hilo la balagha kwa lengo la kutafuta ushahidi au taarifa mpya bali analitumia ili kumwelekeza mlalamishi kuhusu jambo analoliona kuwa wazi. Hili linaimarishwa na kauli ya wakili anaposema, *'Wewe ndiwe umeleta kesi hii mbele ya mahakama.'* Usisitizaji huu wa hoja ni mbinu ya wakili ya kumwelekeza mlalamishi katika jibu analotarajia.

Isitoshe, Swali balagha la wakili la *'Hujui hata mmoja mwenye umeshitaki kwa hii kesi?'* lina dhima ya kuonyesha ukinzani katika kauli za mlalamishi ambaye anadai kutowafahamu watu aliokuwa ameshitaki katika kesi hii.

Vilevile, matumizi ya maswali balagha yalitumika katika mazingira tofauti ya matumizi ya lugha kama inavyoonekana katika dondoo lifuatalo:

> *Wakili: Si utumie Kiswahili? Hii shamba ilikuwa imesajiliwa kwa jina la marehemu X? X ni nani kwako?*
> *Mlalamishi: Ni ndugu yangu.*

Hapa, swali *'Si utumie Kiswahili?'* ni swali balagha linalotumika baada ya mshiriki kutumia lugha ya Kiluo. Muundo wa kukanusha *'si'* anaotumia wakili unalifanya swali hilo kuwa elekezi hivi kwamba mlalamishi alihitajika kutumia lugha ya Kiswahili. Hivi, dhima ya swali hili si kutafuta tu taarifa bali kumshurutisha mlalamishi kubadili lugha ya mawasiliano na kurejea kwenye lugha inayokubalika. Tofauti na matokeo ya utafiti wa Alkabiri (2024) aliyeyaona maswali balagha kama zana za ushawishi mahakamani, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa ushawishi baina ya wahusika mahakamani hutekelezwa kupitia mikakati ya mawasiliano ambapo hususan mawakili hutumia maswali balagha kusisitiza umbali wa kimawasiliano baina yao na washiriki wengine. Jambo hili linathibitishwa kwa misingi ya Fairclough (1989) ambaye haitazami lugha kama chombo cha kuleta ushawishi katika jamii bali kama uwanja ambamo wenye mamlaka kama mawakili, hujitenga na kuonyesha utofauti wa kimamlaka na walio chini yao.

Kwa kuzingatia nadharia ya Ujihusishaji (Giles et al., 1991) matumizi ya maswali balagha katika dondoo za mawasiliano haya zinaelekea zaidi katika mawasiliano ya ujihusishaji wa mwachano. Ujihusishaji huu wa mwachano unaweza kuelezwa kwa kuzingatia vipengele vya lugha na utambulisho vya nadharia hii. Kwamba, matumizi ya lugha ya Kiluo na mlalamishi yanageuka na kuwa kichocheo cha utengano wa kimawasiliano baina yake na wakili na kuishia kujitenga na mazingira magumu katika mawasiliano yale.

Isitoshe, badala ya wakili katika mfano wa pili kujaribu kupunguza tofauti za kimawasiliano baina yake na mlalamishi anatumia maswali balagha kusisitiza msimamo wake na hivi kumweka mshiriki katika nafasi ya kukubali tu msimamo huu. Hili linabainika wakili anaposisitiza kupitia swali *'Si utumie Kiswahili?'* kama njia ya kumlazimisha mlalamishi kutumia lugha ambayo ingewawezesha kukutana. Hali hii inaweza

kufafanuliwa kama ujihusishaji wa mwachano kwa kutumia kipengele cha utambulisho cha nadharia hii wakili analenga kusisitiza utambulisho wake wa kitaasisi na kimamlaka katika muktadha huu mahakamani.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Utafiti huu umebaini kuwa mbinu za kuchanganya na kubadili lugha, takriri na maswali balagha zilitumika ndani ya mikakati ya mawasiliano hususan maswali, mazungumzo na mahojiano katika mawasiliano kwenye mahakama ya Juu ya Mazingira na Ardhi ya jiji la Kisumu. Matokeo yamebainisha kuwa mbinu hizi za lugha hazikutumika tu kwa madhumuni ya kupata taarifa pekee bali zilitumika kama vichocheo vilivyosukuma matumizi ya mikakati hiyo ya mawasiliano ili kuwawezesha washiriki kukidhi malengo yao ya mawasiliano mahakamani.

Vipengele vya lugha, muktadha na utambulisho vya nadharia ya Ujihusishaji vilidhihirisha namna mahusiano ya kimamlaka yalivyoathiri uchaguzi wa mbinu hizi huku wahusika wakijihusisha kwa kuachana ama kwa kukutana.

Matokeo yanaonyesha kwamba mbinu za kuchanganya na kubadilisha lugha pamoja na takriri ziliwawezesha washiriki kukutana kimawasiliano na hivyo kurahisisha mtiririko wa mazungumzo. Kinyume chake ni kwamba mbinu ya maswali balagha ilisababisha umbali wa mawasiliano baina ya mawakili na walalamishi. Utafiti vilevile umeonyesha kuwa uchanganuzi wa mbinu za lugha hauwezi kutenganishwa na mikakati ya mawasiliano katika muktadha huu kwa kuwa mwingiliano wa vipengele hivi ndio unaoeleza namna mawasiliano ya kimahakama hujengwa na kuelekezwa.

Mapendekezo: Hivyo, matumizi ya mbinu za lugha zinazoimarisha maelewano, ushirikiano na mawasiliano yenye ufanisi kupitia kwa mikakati tofauti ya mawasiliano yanapaswa kupewa kipaumbele katika mawasiliano mahakamani. Isitoshe, utafiti huu unapendekeza kwamba mahakama ishirikiane na wataalamu wa Isimu ili wasomi wa taaluma ya kisheria hususan majaji na mawakili waweze kupewa mafunzo kuhusu mbinu za kuchanganya na kubadili lugha, takriri na maswali balagha; ili kuwawezesha kutambua na kuzitumia ipasavyo katika mawasiliano mahakamani.

MAREJELEO

Alkabiri, M. A. (2024). Argumentation strategies in courtroom discourse. *World Journal of English Language, 14*(2), 366–377. https://doi.org/10.5430/wjel.v14n2p366

Aldosari, A. (2023). Rhetorical strategies of legal arguments in courtrooms. *Theory and Practice in Language Studies, 13*(7), 1689–1697. https://doi.org/10.17507/tpls.1307.12

Binyanya, R. M. (2014). *Sajili ya maafisa wa polisi: Tathmini ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kituo cha polisi cha Central, Nairobi* [Master's thesis, University of Nairobi].

Cotterill, J. (2003). *Language and power in court: A linguistic analysis of the O. J. Simpson trial*. Palgrave Macmillan.

Drew, P., & Heritage, J. (Eds.). (1992). *Talk at work: Interaction in institutional settings*. Cambridge University Press.

Fairclough, N. (1989). *Language and power*. Longman.

Gibbons, J. (2003). *Forensic linguistics: An introduction to language in the justice system*. Blackwell Publishing.

Giles, H., Coupland, J., & Coupland, N. (1991). Accommodation theory: Communication, context and consequence. In H. Giles, J. Coupland, & N. Coupland (Eds.), *Contexts of accommodation: Developments in applied sociolinguistics* (pp. 1–68). Cambridge University Press.

Hautli-Janisz, A., Budzynska, K., McKillop, C., Pluss, B., Gold, V., & Reed, C. (2022). Questions in argumentative dialogues. *Journal of Pragmatics, 188*, 56–79. https://doi.org/10.1016/j.pragma.2021.10.029

Heffer, C. (2005). *The language of jury trial: A corpus-aided analysis of legal-lay discourse*. Palgrave Macmillan.

Kiguru, G. (2014). *A critical discourse analysis of language used in selected courts of law in Kenya* [Master's thesis, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/14017

Nabirye, N. (2012). *Language strategies in interaction: A study of repetition, lexical choice and hedging in discourse* [Unpublished master's thesis, Makerere University].

Obange, N., & Wagah, G. G. (2019). Land tenure challenges in Kisumu City, Kenya. *Net Journal of Social Sciences, 7*(4), 85–91. https://doi.org/10.30918/NJSS.74.19.023

Omwancha, J. K., Odhiambo, K., & Ombati, J. (2024). An analysis of representative speech acts in selected subordinate courts of law in Kenya. *International Journal of Literature, Language and Linguistics, 7*(3), 57–72. https://doi.org/10.11648/j.ijll.20241206.13

Owiti, B. (2016). *Courtroom interpretation from Dholuo to English: A stylistic and pragmatic analysis* [Doctoral thesis, University of Huddersfield]. University of Huddersfield Repository. https://eprints.hud.ac.uk/id/eprint/30239/